Mlalamikaji lazima afike kusikiliza shauri la sivyo amri hiyo ya dharura itatupiliwa mbali moja kwa moja. Mshtakiwa hahitajiki kufika kwa usikilizaji wa mwisho. Ikiwa mshtakiwa hatofika kwenye usikilizaji bado mahakama inaweza kutoa amri ya RFA. Amri ya mwisho haifanyi kazi hadi pale mshtakiwa amefikishiwa.

Ikiwa baada ya kusikiliza ushahidi wote jaji akaamua kuwa hakuna ushahidi wa kutosha kutoa amri ya mwisho, amri ya dharura itakoma na shauri litafungwa.

## Msaada wa Mwisho kuondokana na Amri ya Ulinzi dhidi ya Unyanyasaji

Mlalamikaji na mshtakiwa wote watapewa nakala ya amri hiyo. Ikiwa mshtakiwa hayupo kwenye usikilizwaji shauri vyombo vya sheria vitamfikishia mshtakiwa nakala. Ikiwa jaji atatoa amri ya mwisho lazima iwe kwa muda maalum.

Kabla ya amri ya mwisho kumalizika muda wake mlalamikaji anaweza kuwasilisha ombi kwa maandishi mahakamani ili amri iongezwe muda. Nyaraka hizi zinapatikana kwenye mahakama hizo, chama cha utetezi cha eneo lako na katika www.vermontjudiciary.org.

## Ukiukaji wa Amri ya Mwisho

Ni kosa kukiuka amri ya RFA. Ikiwa mshtakiwa atafanya jambo ambalo amri inasema hawezi kufanya, unapaswa kuita vyombo vya sheria; vyombo vya sheria vinaweza kumkamata mshtakiwa.

**Nambari ya kupiga simu kwa amri ya RFA wakati mahakama zimefungwa:**

**1-800-540-9990**

**Msaada Unaopatikana**

**Nambari ya Simu ya Ukatili Majumbani**

**1-800-228-7395**

Unaweza kupiga simu na kuuliza nambari ya simu ya kikundi cha utetezi dhidi ya ukatili wa majumbani au tembelea wavuti huu https://vtnetwork.org/get-help/

Tovuti ya Mahakama:

**www.vermontjudiciary.org**

## Kusajili kesi ya Msaada kutoka Amri ya Unyanyasaji katika Mahakama ya Familia

Kijitabu hiki kitakusaidia kuelewa jinsi sheria inavyofanya kazi kwa Msaada wa Amri dhidi ya Unyanyasaji (RFA). Tafadhali soma kijitabu hiki chote kabla ya kufungua shauri la amri ya RFA. Mtu anayeomba msaada wa amri dhidi ya unyanyasaji ni “mlalamikaji”. “Mshtakiwa” ni mtu ambaye unaomba amri dhidi yake. Sio lazima uwe raia ili kufungua shauri. Hakuna ada ya kusajili kesi au gharama.

Amri ya RFA ni amri iliyotolewa na jaji wa mahakama ya familia ili kukulinda wewe na/au watoto wako dhidi ya mshtakiwa.

Kijitabu hiki kinatoa maelezo mafupi tu. Unaweza kuhitaji kuzungumza na wakili.

**Mahakama ya Vermont Mtandaoni**

www.vermontjudiciary.org

## Jinsi ya kusajili Amri ya RFA :

Unaweza kusajili Amri ya Dharura au Isiyo ya Dharura ya RFA muda wa saa za mahakama. Usajili wa dharura unaweza kufanywa wakati wowote mchana au usiku.

Ili kusajili amri ya RFA lazima uonyeshe kuwa mshtakiwa ni mmojawapo wa wafuatao:

- Mwanafamilia
- Mwanakaya
- Mke/mume wa sasa au wa zamani
- Mtu ambaye umewahi kuishi naye
- Mtu ambaye umewahi kutoka/kuchumbiana naye
- Mtu ambaye umekuwa na uhusiano wa kimapenzi naye au kushiriki ngono

*Ikiwa uhusiano wako na mtuhumiwa haupo katika yoyote ya hapo juu, unaweza kustahili kusajili amri dhidi ya Unyemeleaji au Ubakaji. Unaweza kuchukua kijitabu cha Unyemeleaji au Ubakaji mahakamani au www.vermontjudiciary.org .*

Na ni lazima pia uonyeshe kwamba:

- Mshtakiwa alikudhuru kimwili
- Mshtakiwa alijaribu kukudhuru
- Mshtakiwa alikuweka katika hofu ya madhara makubwa ya mwili
- Na unaogopa kwamba mshtakiwa atakudhuru, au atakuweka katika hofu ya madhara makubwa ya mwili siku za usoni

Utahitaji kujaza fomu ya malalamiko na uandike hati ya kiapo. Jaji atapitia shauri lako siku hiyo hiyo lilipowasilishwa. Kulingana na shauri lako, jaji atatoa au kukataa ombi lako la Amri ya Dharura ya RFA.

## Ikiwa ombi lako la Amri ya Dharura Limekataliwa

Unaweza kuomba usikilizaji wa mwisho juu ya shauri lako. Utakuwa na nafasi ya kutoa ushahidi mahakamani kujaribu kuthibitisha shauri lako. Ikiwa utaomba kusikilizwa, basi malalamiko yako, hati ya kiapo na ilani ya kusikiliza shauri itatumwa kwa vyombo vya kisheria. Kisha vyombo vya kisheria vitamfikishia nyaraka hizo mshtakiwa kwa mkono. Ukiamua kutokuomba kusikilizwa kwa mara ya mwisho, malalamiko yako na hati ya kiapo itahifadhiwa kwa siri na mshtakiwa hatoweza kupata nakala ya usajili wa dharura uliowasilisha.

## Ikiwa Ombi la Amri yako ya Dharura Limekubaliwa

Amri ya dharura iliyotolewa na jaji ni agizo la muda tu, inatumika hadi usikilizwaji wako wa mwisho. Usikilizaji wa mwisho utapangwa kati ya siku kumi za kazi baada ya kusajili. Wakati wa kusikilizwa, wewe na mshtakiwa mtaweza kumweleza jaji kile kilichotokea na kuleta mashahidi watoe ushahidi.

Jaji anaweza kuagiza yoyote yafuatayo kwa bila kukufahamisha awali:

- Mshtakiwa aache kukunyanyasa wewe na/au watoto wako
- Mshtakiwa aache kukusumbua wewe na/au watoto wako
- Mshtakiwa akae mbali na wewe, watoto wako, nyumba yako, mahali pako pa kazi, gari lako
- Mshtakiwa asiwasiliane na wewe au kuruhusu tu aina fulani za mawasiliano
- Mshtakiwa aondoke nyumbani kwako kwa muda
- Una ulezi wa muda wa watoto

**Mahakama itatuma nakala ya malalamiko yako, hati ya kiapo na amri ya muda, na tarehe ya kusikilizwa, kwa vyombo vya kisheria na itatoa nakala kwa mshtakiwa.** Hadi pale vyombo vya sheria vitakapofikisha nyaraka amri ya muda haitafanya kazi.

Hakikisha unapata nakala yako ya amri kutoka mahakamani. Tarehe na saa ya usikilizaji shauri lako iko kwenye ukurasa wa pili wa amri.

## Nini cha Kutarajia Katika Usikilizaji wa Mwisho wa Kesi

Kwenye mkutano wa mwisho wa RFA mlalamikaji na mshtakiwa watapata nafasi ya kutoa ushahidi. Pia, kila mmoja anaweza kuleta mashahidi kutoa ushahidi. Mlalamikaji anaweza kuomba amri itolewe kwa kipindi maalum.

3/2021